


PROGRAMU YA KUFUNDISHA KIINGEREZA KWENYE MENASHA HIGH SCHOOL

Kuhudumia Wanafunzi wa lugha nyingi katika muundo unaojumisha na jumuishi

DARASA ZENYE KUFUNDISHWA NA WALIMU WAWILI

Wanafunzi katika Programu ya EL wanachukuaga madarasa za sanaa ya lugha, hesabu, sayansi na masomo za kijamii. Somo hizi zinafundishwa vizuri na mwalimu wa darasa hilo pamoja na Mwalimu wa Mwanafunzi wa Kiingereza katika darasa la pamoja.



MAENDELEO YA LUGHA YA KIINGEREZA

Wanafunzi huondoka kwenye Programu ya EL baada yakupata kiwango cha 5 kwenye Jaribio la ACCESS, ambalohupima lugha ya kitaaluma ya kiingereza. Maendeleo ya lugha ya Kiingereza kwa wanafuzi wetu inatokea kwa kufundishwa na walimu wawili, Programu ya TWI na kwa Darasa la Maendeleo ya Lugha ya Kiingereza haswa kwa wanafunzii wapya inchini.

WASIMAMIZI WA KESI ZA EL

Wanafunzi kwenye Programu ya EL huwa na walimu wenye kuhudumia kesi zao. Wasimamizi wa kesi hufanya kazi na mwanafunzi, walimu wa mwanafunzi na familia ya mwanafunzi kwa kusaidiana kuelewa maendeleo ya lugha na mahitaji zingine za mwanafuzi kwa kumusaidia aweze kufaulu shuleni.



PROGRAMU YA KUFUNDISHA KWA NJIA YA LUGHA MBILI

Kupitia madarasa zetu zilizofundishwa, sisi tunatoa mipango ya lugha mbili kwa kukuza lugha ya masomo ya wanafunzi kwa kusoma na kuandika katika Kihispania na kiingereza. Madarasa zinafundishwa katika masomo za kijamii na Lugha ya Ulimwengu ya Uhispania wakati wamiaka ya freshmen na sophomore.

